MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na: 16. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Machi 1-10, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Machi 11-20, 2019**

**Muhtasari**


- Wakulima katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wanaendelea na shughuli za palizi na uwekaji wa mbolea
- Wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua wanaendelea na kuandaa mashamba na kupanda
- Wakulima , wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuendelea kufatilia tabiri za hali ya hewa na ushauri. Pia wapate ushauri wa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya mvua zinazotarajiwa katika maeneo yao.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2019

Katika kipindi hiki migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Hali hii iliendelea kusababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kubaki kusini katika nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani liliendelea katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hali iliyosababisha kutokea kwa vimbunga. Joto la bahari la wastani liliendelea katika eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ilipelekea upepo kuvuma kutoka magharibi hivyo kuimarisha mifumo ya mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2019

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua za zaidi ya milimita 25. Kiwango cha juu cha mvua ya zaidi ya milimita 100 zilipatikana katika maeneo ya mikoa ya Morogoro, Njombe, Ruvuma na Mtwara. Hata hivyo, maeneo machache kuzunguka ukanda wa kaskazini mashariki na kaskazini mwa mkoa wa Tanga yalipata mvua kidogo (chini ya milimita 10) kama inavyoonekana kwenye kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Machi 1- 10, 2019

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2019

Katika kipindi cha siku kumi (dekadi) zilizopita, mahindi katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua yalikuwa katika hatua ya kutoa mbelewele na kubeba. Kwa ujumla mazao yalikuwa katika hali nzuri. Wakulima katika maeneo hayo wameendelea na shughuli za palizi pamoja na uwekaji wa mbolea. Kwa Upande mwingine wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua wanaendela na kuandaa mashamba na kupanda. Hali ya upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo ilikuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu unayoendelea

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWAKATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kudhohofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kusogea kidogo kuelea kaskazini mwa kusini mwa nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi hali inayotarajiwa kusababisha kutokea kwa vimbunga. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii haitarajiwi kusababisha mabadiliko makubwa ya mifumo ya hali ya hewa

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2019

Katika kipindi cha siku kumi zijazo **Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), Nyanda za juu Kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) na Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi)** inatarajiwa kuwa na mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja** na Pemba) inatarajiwa kuwa na Mvua katika baadhi ya maeneo.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro)** inatarajiwa kuwa na mvua katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida)** inatarajiwa kuwa na mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20,2019

Mvua zinazotarajiwa katika siku kumi zijazo zitaendelea kuongeza unyevunyevu kwenye udongo hususan katika maeneo mengi yanayopata mvua za msimu mmoja kwa mwaka na kuwezesha ukuaji mzuri wa mazao na pia kusaidia upandaji, ukuaji wa mbegu katika maeneo yanayopata mvua za misimu miwili kwa mwaka. Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuzitumia mvua hizi za msimu na masika ipasavyo ikiwa ni pamoja na kupata ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao ili kupata tija katika shughuli zao.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2019.

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu hususan maeneo ambayo huwa yanakabiliwa na upungufu wa maji.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

*S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz*